HAWA NI vijana wanaojulikana kama Kamiti Tanners FC kutoka Nairobi. Ni wanandinga mashujaa ambao wameanza kujitokeza na kuonyesha mbinu za kulisakata kandanda. Katika michuano yao ya hivi karibuni, walipambana na miamba ya Mombasa, Nyundo FC na kufungwa 4-0 lakini wanasema, "tumejifunza na tutashinda siku nyingine".

Majenzi Yote Ya Misikiti Yakamilishwe — Mwidani

na Abdulrahman Sheriff

MEYA WA Mombasa, Diwani Ahmed Shahame Mwidani alihuzunishwa na uchelewaji wa kukamilishwa kwa majenzi ya Misikiti na akatoa ombi kwa Waislamu wote kote nchini watimize wajibu wao wa kuona Miskiti yote yamemalizwa kujengwa.

Akihutubia kwenye Harambee kubwa ya kuchangia ujenzi wa Msikiti wa Shakombo katika Mtongwe Vijiweni, Meya Mwidani aliwasihi Waislamu wauchangie Msikiti huo hadi utakapokamiika na Waislamu wa sehemu hiyo wapate kufanya ibada zao.

Diw. Mwidani aliwasihi Waislamu waache utesi katika Misikiti na wasihubiri fitina ama kugombana wenyewe kwa wenyewe. "Waislamu wanahitajika kushirikiana na kuonyesha umoja wao ambao utakuwa mfano mwema kwa vijana wanaoinukia", akasema.

Akihutubia kwenye mkutano huo, Mwenyekiti wa Kana wilayani Mombasa, Bw. Sheriff Nassir aliwaomba Waislamu waiheshimu Serkali kama vile Serkali inavyoheshimu dini ya Kiislamu. "Ingawa Waislamu tuko wachache nchini, Serkali imetupa Uhuru wa kujifanya mambo yetu bila kutuingilia", alisema Bw. Nassir.

Bw. Nassir aliye pia Mbunge wa Mombasa ya Kati na Waziri Mdogo wa Ardhi na Makao aliongeza kuwaambia waliohudhuria kuwa Waislamu hawafai kuteta, kutukanana ama kutetea mambo ya dini na akawaomba wasitoe khitilafu ya dini yao nje.

MWENYEKITI wa Kanu wilayani, Bw. Sheriff Nassir akipokea mchango kutoka kwa Meya wa Mombasa, Diwani Mwidani.

MAMLAKA

Mwenyekiti huyo alisifu maongozi ya Serkali ya kutoa mamlaka kila mtaa na wilaya ijitanyie mambo yao ya maendeleo na kumaliza matatizo yao wenyewe. "Wananchi wamepewa Uhuru mkubwa wa kujichagulia mambo wanayoyataka na kuyatekeleza bila kuingiliwa", akaongeza.

Mwenyekiti wa Kanu wa Mombasa Kusini, Bw. Mbaruk Bandari alisifu umoja ulioko Mombasa tangu kumalizika kwa uchaguzi wa Kanu na akawashuri viongozi wote washirikiane katika kutekeleza miradi mbali mbali ya maendeleo katika wilaya ya Mombasa.

Bw. Bandari alikariri umuhimu wa viongozi kuheshimu chama cha Kanu na akawataka Madiwani na Wabunge washirikiane na viongozi wa Kanu katika harakati za kuwatumikia wananchi katika mambo ya maendeleo na kuwaondolea matatizo yanawakabili.

Mkutano huo pia ulihutubiwa na Mbunge wa Mombasa Kusini, Bw. Abdallah Ndovu Mwidau, Mbunge anayewakilisha sehemu hiyo ambaye aliwataka Waislamu wapendane. " Mwenye-Ezi-Mungu hapendi Mwislamu kumyamazia mwenzake anapomsalimu", akasema Bw. Mwidau.

Jumla ya 164,361/70 zilikusanywa kwenye Harambee hiyo ambapo Mgeni wa Heshima, Bw. Nassir alitoa 12,400/-, Bw. Mwidau 1,000/-, Meya Mwidani 4,401/-, Diwani wa sehemu hiyo, Bw. Hassanali 5,000/- pamoja na saruji tani 8 na kamati ya msikiti huo ikachangisha 104,000/-.

Inasemekana kwamba mpango wa kuchangia Msikiti huo unaendelea lakini haikufahamika kama mkutano mwingine wa Harambee utafanyika kukusanya kiasi kilichobakia kukamilisha majenzi yake. Msikiti huo unategemea kugharimu kiasi cha Shilingi Milioni Nane Unusu (8,500,000/-).

Kwa Heko Diwani Wa Jomvu

BW. ALI NGAO.

NIKIWA mkaazi wa Jomvu Kuu, sina budi kutoa pongezi zisizo na kifani kwa Diwani wa sehemu anayotuwakilisha ya Mikindani, Bw. Ramadhan Kajembe kwa juhudi anazofanya katika kuleta maendeleo kwenye sehemu yetu.

Hapana shaka wala tashwishi kuwa Diwani. Kajembe ameshatekeleza mengi ya manufaa kwetu sisi anaotuwakilisha. Ni juu yetu wananchi wa sehemu hii, tushirikiane naye katika mipango aliyonayo ya kutunufaisha.

Hakika Diwani Kajembe ameshatufanyia mengi ambayo yanaonekana wazi na nina uhakika ameshafanya taratibu nyingine ya kujenga sehemu zetu hizi kutoka Mikindani na hapa Jomvu Kuu na ni juu yetu kushirikiana naye na kumpa nguvu zaidi.

Sina mengi kwa leo isipokuwa nawaomba wananchi wote wasidanganyike na wenye kusema bila vitendo kwani napenda kumalizia hivi, "maneno matupu hayajengi bali yanavunja. Umoja wetu ndio ambao utatuletea manufaa na maendeleo zaidi katika mikindani wadi".

ALI NGAO
MKAZI WA JOMVU KUU

Vazi La Bui Bui

NAPENDA kumuunga mkono Mhariri Wetu, Ndugu Abdulrahman Sheriff kwa maoni yake kuhusu kulazimishwa kwa wasichana wa mashule kuyavua mabuibui na kuomba hatua ichukuliwe kwa waalimu wanaotenda wanaolazimisha jambo hili.

Kiislamu na Kimwambao, vazi la buibui ni sitara kwa wasichana na kwa karne nyingi. Limekuwa likuvaliwa na hawa wanafunzi hawalivai kiholela bali ni kutokana na mafunzo na maamrisho ya dini yao ya Kiislamu.

Ni Jambo la kushangaza kusikia wakuu wa shule wakikataza mabuibui yasivaliwe hali katika mashule hayo, mafunzo ya dini yanasomeshwa. Uislamu unafunza nidhamu na uadilifu kwa vijana wa Kiislamu.

Hakuna Mwalimu asiyemjua mwanafunzi wake na vitambulisho viko, kuwavua mabuibui ni kisingizio kisicho na msingi.

SALIM ALI LIKONI,
MOMBASA.

Na Tifu Naye Awashauri Wana Wa Kanu Watumike

NAIBU MWENYEKITI wa Kanu wadi ya Makadara, Bw. Abdullatif "Tifu" Ubwa amewashauri viongozi wa Kanu wa ngazi zote kujitolea kikamilifu katika harakati za kutayarisha mipango ya maendeleo na kuwasaidia wananchi wa sehemu zao. **(Aripoti Abdulrahman Sheriff).**

Akihutubia mkutano wa Harambee katika Uwanja wa Makadara, kwa ajili ya kumchangia Bi. Zainabu Mohammed Abdallah ambaye atafanyiwa upasuaji wa figo, Bw. Ubwa alisema, "umefika wakati viongozi wa kanu wajitolee kutatua matatizo madogo madogo".

KAZI

Aliongeza kusema kuwa haifai kuwafanyisha kazi viongozi wa ngazi za juu kupita kiasi. "Matatizo madogo madogo twaweza sisi viongozi wa ngazi za chini kuyatatua kwani tunatambulikana tulichaguliwa na wananchi kuwatumikia", akaeleza.

Bw. Ubwa alimpongeza Mwenyekiti wa Kanu wilayani, Bw. Sheriff Nassir kwa juhudi anazozifanya na akawataka viongozi wa Kanu wafuate mfano wake kwa kujishirikisha kikamilifu kwenye mipango na shughuli mbali mbali za ujenzi wa taifa.

Akihutubia kwenye mkutano huo, Bw. Nassir aliye pia Mbunge wa Mombasa ya Kati na Waziri Mdogo wa Ardhi na Makao aliwataka wananchi wajitokeza kwa wingi kila kunapoluwa na mikutano ya mipango ya maendeleo na kuwachangia walio wagonjwa na wenye kwenda ng'ambo kusoma.

Alisema: "Hatuna budi kujishughulisha na kujitolea katika kujenga nchi yetu kwa vitendo kwani wakati wa siasa umekwisha na sasa ni wakati wa kuijenga nchi yetu na hatutaweza kuijenga bila ya kujitokeza na kusikiliza mawaidha ya viongozi"

Jumla ya 114,363/75 zilikusanywa kwenye Harambee hiyo ambapo Bw. Nassir na maafisa wa Kanu walitoa 15,000/-. Bi. Zeinabu Mohammed Abdallah atafanyiwa upasuaji wa figo na mwanaye wa kike amejitolea kumpa mamake figo moja.

MWENYEKITI wa Chama cha Wanafunzi wa Zamani wa Allidinah Visram High School, Bw. Ahmed Bachani (kushoto) akimkabidhi Meya wa Mombasa Diw. Ahmed Mwidani kitabu maalum chenye kumbukumbu ya shule hiyo wakati viongozi na wananchama wa chama hicho walipo mtembelea katika sebelu yake hivi karibuni. Chama hiki kimeazimia kuanzisha miradi kadha ya kusaidia maendeleo ya shule hiyo.

Farucci

BINT EL SUDAN
Perfume • Powder
Pomade • Deodorant

MARASHI
ASILI YA MAPENZI
HAKIKA
UTA FURAHI

JISHINDIE VIATU MARIDADI VYA FARUCCI KWA MSHINDI WA KWANZA NA 'BINT EL SUDAN -

GIFT PACK' KWA MSHINDI WA PILI NA WATATU ATAPATA ZAWADI YA FLANA YA FARUCCI
CROSSWORD No. 221

KWENDA KULIA:

1. Mwizi atumiaye silaha. 5. Medical Officer. 6. Ni mzaa baba kisha ni tunda. 7. Umoja wa mataifa. 8. Namna ya embe. 9. Mnyama mkubwa mwenye umbo kama la paka. 10. Chimba udongo kama vile maji yanavyomomonyoa. 14. Kama No.7 kwenda kulia. 15. Utulivu. 17. Kivazi cha kike. 18. Asili ya tunda. 19. Tosha, pekee.

KWENDA CHINI:

1. Aina ya mdudu. 2. Kinyume cha bandika. 3. Zaidi. 4. Aina ya samaki wa bahari. 5. Wakati. 9. Kidonda kikubwa. 11. Mbaya. 12. Mti wa mtama. 13. Mjinga, mpumbavu. 15. Namna ya karata. 16. Weka ndani. 17. Afrika kusini.

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 220

KWENDA KULIA: 1. KAMBARE, 5. LA, 6. MOMBASA, 9. DA, 10. AMUA, 11. UKAKASI, 13. KESI, 14. GUU, 16. UTU, 18. AM, 19. PANDA, 21. ALA, 22. TII. *KWENDA CHINI:* 1. KIMBUNGA, 2. BABAKE, 3. RISASI, 4. MAKANJU, 7. MDAKU, 8. AMI, 12. ASIA, 15. UMA, 16. UDI, 17. TAI, 19. PA, 20. NT.

WASHINDI WA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 220

AMINA KANDIE, Sanduku La Posta 93044, Mombasa. 2. FRANCIS KALAITA MUNYALO, Sanduku La Posta 83987, Mombasa. 3. AHMED MOHAMED, Sanduku La Posta P.O. Box 81412, Mombasa.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Kila baada ya wiki mbili, Mshindi wa kwanza atapata viatu maridadi vya Farucci; wa pili atapata 'Bint El-Sudan-Gift Pack' na watatu atajinyakulia flana ya Farucci. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK* Limited Mombasa. Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Mhariri *COASTWEEK*, S. L. P. 87270, Mombasa. Mwisho wa kutuma Majibu na jumatano, **Desemba 11, 1985** saa, nne asubuhi.



JINA.............................

SANDUKU LA POSTA.....................